



## Maswali na Majibu

1. Imani ni nini?  
*Kuwa na ukweli kwa mambo tunayotumainia na kutarajia vitu tusivyoviona.*
2. Lazima tuamini nini ili tumpendeze Mungu?  
*Kwamba Mungu yuko na huwazawadisha wamtafutao.*
3. Tunakuwa na imani namna gani?  
*Kwa kuomba na kusoma neno la Mungu.*
4. Usaizidi wa nani utatusaidia tuwe na imani?  
*Tunahitaji usaizidi wa Mungu.*
5. Mbona tusiwe na wasiwas?  
*Mungu ako kila siku na anatujali. Anataka tuwe kwa Ufalme Wake. Anajibu maombi yetu na kutupa nguvu ya kukabiliana na shida.*
6. Nini ilifanyika Sauli alipokosa imani? Nini ilifanyika Daudi alipokuwa na imani?  
*Sauli hakutii Mungu. Daudi aliua jitu Goliathi.*
7. Dhahabu husafiswa namna gani? Nasi hujaribiwa namna gani ili tuwe sawa?  
*Dhahabu husafiswa kwa moto. Sisi hujaribiwa kwa shida zetu.*
8. Tunaonyesha imani yetu kwa maisha haya namna gani?  
*Kwa kumtii Mungu na kuwa na upendo Wake.*
9. Ibrahimu na Rahabu walionyesha imani yao namna gani?  
*Ibrahimu alikuwa tayari kumtoa mwanawe. Rahabu alificha wapelelezi.*
10. Watu waliotajwa kwa Waebrania 11 wanasaidia imani yetu namna gani?  
*Ni kama kundi la watu wanatuhimiza kwa mfano wao.*

## Mistari ya kukariri

Waebrania 11:1   Waebrani 11:6   Waebrania 12:2   Waefeso 2:8

## Mazungumza

Zungumza vile unaweza kuwa na imani. Jadiliana vile kila mmoja wenu ameomba juu ya nini na vile Mungu amejibu hayo maombi. Amekusaidije kwa shida na majaribu.

## Kuandika

Chagua watu 3 kutoka kwa Waebrani mlango wa 11 na uandike vile walionyesha imani yao.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 20   Imani na utiivu

### SOMA   Waebrania mlango wa 11 mpaka mlango wa 12:2

#### SOMO

Imani ni nini? Biblia inatuelezea kwa Waebrania 11:1, "Imani ni kuwa na uhakika ya mambo yatarajiwayo tena na kwa mambo yasionekana."

Kuna msemo usemwao, "Kuona ndiyo kuamini au Nitaamini nikiona." Sote tunaamini kwa vitu tunavyoviona kila siku. Ingawaje ni vigumu kuamini kwa vitu tusivyoviona. Tumaini ni kutarajia vitu vizuri kufanyika. Imani ni kuwa na ukweli kwamba vitafanyika. Tunatakiwa kuwa na imani ili tuamini kwa Mungu na Wokovu wake.

Waebrania 11:6 inasema, "Bila imani ni vigumu kufurahisha Mungu kwa sababu kila amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeeye yuko na huwapa thawabu wale wamtafutao."

Huu ni mstari wa maana sana. Unasema kwamba ni vigumu kumpendeza Mungu kama hatuna imani kwake na kwa ahadi za wokovu. Ni rahisi kuamini kwa vitu tunavyoviona. Lakini tujue kwamba vitu hivi vyote vitabadilika, vitachakaa au vitakufa. Mungu ni wa milele, wa uwezo wote kutoka mwanzo hata mwisho. Ni wa ukweli zaidi kuliko vyote tunavyoona. Mungu hawezikudanganya kwa hivyo ahadi zake zote zitatimizwa.

Kwa hivyo tunaweza kuwa na imani namna gani? Kuamini Mungu na ahadi zake lazima tusijue. Kujifunza juu ya Mungu na ahadi zake tunapaswa tuombe Mungu atusaidie na tusome neno Lake, Biblia. "Imani huja kwa kusikia, na kusikia neno la Mungu." Warumi 10:17. Tunapaswa kulisikilize neno la Mungu – tulisome na tulitafakari. Maneno tunayoyasikiliza yanaweza kugeuza tunayofanya. Tukizikiliza mambo ya ulimwengu hatutakuwa na imani. Neno la Mungu liko kama mbegu yenye inapandwa ndani ya miyo yetu na inazaa imani kwetu. Inatupidi tuwe na imani hii kutoka kwa neno la Mungu.

Tunastahili kuwa na ukweli kwamba Mungu hutimiza ahadi zake. Tumwamini kabisa na tulikubali neno lake katika miyo yetu. Imani itatufanya tujue miyoni mwetu kama tunaona kwa macho. Tunapaswa tuenende kwa imani sio kwa kuona. 2 Wakorintho 5:7


Ni vigumu kumpendeza Mungu kama hatuna imani. Uhusiano wetu na Mungu unategemea imani yetu. Imani ni jambo la milele. Kuwa na imani tunahitaji usaizidi wa Mungu. Waefeso 2:8 inatwambia, "Maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani – ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu." Lazima tuwe na imani kwa neema ya Mungu, lakini hata hiyo neema kutoka kwa Mungu na ni kipawa Chake. Hatuwezi kuwa na imani sisi wenyewe bila usaizidi wa Mungu.

Imani huleta Mungu ndani ya maisha yetu. Lazima tusijipendeze sisi wenyewe lakini tumpendeze na tumtii Mungu. Imani inamaanisha unategemea kitu. Imani kwa Mungu inamaanisha unategemea Mungu na unaamini kwamba Mungu ni mkuu na anatupenda sana. Mungu anategemewa kila wakati. Anajua tunacho hitaji na anataka kuzitimiza. Mungu anataka tuwe kwa Ufalme Wake. Atatuongoza kwa maisha yetu kwa safari ya kwenda kwa Ufalme Wake.

Mungu huwa karibu na sisi kila siku. Atajibu maombi yetu wakati wote. Lakini kila wakati tuende na mapenzi ya Mungu wakati tukiomba. Wakati tunaomba tunafikiri tunajua kile tunaomba na Mungu atajibu vile TUMETAKA. Kusudi la Mungu ni kutuelekeza kwa Ufalme Wake kwa hivyo jibu lake kwa maombi yetu sio vile tunatarajia. Wakati mwagine jibu la Mungu ni La – lakini hutupa nguvu ya vile tutakabiliana na hayo mahitaji.

Uoga na wasiwasi huthihirisha kukosa imani. Yesu alitwambia tusiogope (soma Mathayo 6:25 – 26). Ni lazima tuwe na imani kwa Mungu na tuamini kwamba atatusaidia kwa majoribu na kwa shida. Mungu ametuahidi kwamba kila jambo linatendeka kwa mapenzi Yake kwa wale wanaompenda. Warumi 8:28. Majoribu katika maisha yetu yaliyomagumu kwa sisi kusitahimili ni Mungu anatuletea ili atujenge na tumwamini na imani. Mungu huwa ndiye muelegezi. Anajua ni nini inatufaa zaidi. Tusiwe na wasiwasi, tumwachie shuguli zote. Imani kwa Mungu inatupa amani. Tunaweza, 'acha na tumwachie Mungu.'

Wakati wanafunzi na Yesu walikuwa kwa mashua, kulikuwa na dhoruba kwa bahari. Mashua ilikuwa inazama. Wanafunzi waliamsha Yesu awasadie. Yesu alizungumza na bahari ikatulia. Yesu aliuliza wanafunzi, "Mbona mlikuwa na uoga? Wapi imani yenu?" Kila mara Mungu na Yesu huwa karibu kutusaidia. Hatutakiwi tuwe na uoga. Inatakiwa tuwe na imani. Tukiwa na Yesu kwa mashua tuwe na furaha na tuchekellee dhoruba yejote!



Tusipoamini kwa Mungu, tunamchukua kwamba yeje ni Muongo. Mungu ako kila pahali na anaona kila kitu. Anaumia tukijifanya kama Hayuko. Anaumia tusipoamini kwa mambo aliyoituahidi. Bila imani hakutakuwa na utiifu. Bila imani kwa ahadi za Mungu hatutafanya kabisa Anayosema. Machoni pa Mungu, kutotii ni uasi. Ni madharau kwa Mungu.

Wakati Sauli alikataa kumtii Mungu na akatoa dhabihu, ni kwa sababu hakuwa na imani. Alikuwa na ugumu sana. Wafilisti walikuwa wanataka kumshambulia na watu wake walikuwa wanamtoroka kwa kuogopa. Lakini Sauli angeamini tu kwamba Mungu anaweza kukuokoa hata na wachache. Kwa hivyo Sauli hakuwa na imani, hakutii Mungu. Imani ya Daudi ilikuwa kuu kiaje? Kwa ajili ya kuwa na imani kwa Mungu, aliua jitu Goliathi.

Kukiwa na imani ya kweli kutakuwa na vitendo vitakavyothibitisha. Huwa tunazungumza na tunafanya vile tunaamini. Imani ya kweli ni zaidi ya dhahabu. 1 Petro 1:7. Dhahabu husafishwa kwa moto. Hata nasi tunasafishwa kwa kujaribiwa kwa shida na ugumu wa maisha. Tunapaswa tutii Mungu tukigeuzwa na shida za maisha.

Yakobo 2:20 – 26. Inatwambia kwamba bila imani kazi yote imekufa. Inatupa mfano wa Ibrahim alipotaka kumtoa mwanawе wa pekee, Isaka kwa sababu alijua Mungu atamfufua awe hai tena. Hata Rahabu alikuwa na Imani kwa Mungu wa Israeli alipoficha wapelelezi wawili. Aliokolewa kwa sababu ya imani yake. Inatulazimu tuwe na imani kwa Mungu tukiishi na kumtii na kufanya kazi kwa upendo. Habakuki 2:4. Inatwambia kwamba waliohaki wataishi kwa imani. Imani ni hali ya maisha.

Waеbrania 11:33 – 37. Inatwambia mambo yenye baadhi ya watu wa Mungu wenye imani walipitia. Mungu aliokoa wengine lakini wengine walikufa kwa ajali ya imani yao. Watapata urithi Yesu akirudi. Mungu aliahidi kwamba hata nasi pia, tutarithiswa katika Ufalme Wake tukiishi kwa imani. Mistari ya 39 na 40.

Waеbrania 11 inatwambia juu ya imani ya watu wa Mungu zamani za kale. Hawa watu wa zamani hawakuamini tu, ila walitenda. Walimfanya Mungu kazi kwa sababu walikuwa na imani Kwake. Mlango wa 12:1 na 2 inatwambia kwamba walikuwa kama kundi la watu katuonyesha sisi mfano vile tunastahili kuishi maisha ya imani kwa Mungu. "Tunapaswa kukaza macho yetu kwa Yesu, kwa yeje imani yetu inategemewa kutoka mwanzo mpaka mwisho."